**Editon Consortium Journal of Kiswahili [ISSN: 2663 -9289]**



**Issue no:** 01 | **Vol no:** 07 | **September** 2026: 147-155

# Uchanganuzi wa Maudhui Kihalisia katika Nyimbo Teule za *Ohangla* za Prince Indah Nchini Kenya

**Millicent Apondi Oloo** [(1)]
**Harrison Onyango Ogutu** [(2)]
**Mary Malenya** [(3)]

(1.2.3) Catholic University of Eastern Africa, Kenya.
Main author's email: olooapondi3@gmail.com

**Article History**
Received: **2026.07.05**
Accepted: **2026.08.17**
Published: **2026.09.23**

**Cite this article in APA**
Oloo, M. A., Ogutu, H. O., & Malenya, M. (2026). Uchanganuzi wa maudhui kihalisia katika nyimbo teule za *Ohangla* za Prince Indah nchini Kenya. *Edition consortium journal of Kiswahili*, *7*(1), 147–155. https://doi.org/10.51317/nn48wq83

**Abstract**
Makala hii inalenga kubainisha maudhui yanayojitokeza katika nyimbo teule za *Ohangla* za Prince Indah na namna yanavyoakisi uhalisia wa maisha ya jamii ya Waluo. Ingawa *Ohangla* ni mojawapo ya aina maarufu za muziki wa asili nchini Kenya, maudhui ya nyimbo zake za kisasa, hususan za msanii mmoja, hayajapata uchunguzi wa kina wa kitaaluma. Makala hii inalenga kubainisha maudhui yanayojitokeza katika nyimbo teule za *Ohangla* za Prince Indah na namna yanavyoakisi uhalisia wa maisha ya jamii ya Waluo. Kwa kutumia Nadharia ya Uhalisia, hasa Mhimili wa Uhalisia wa Maisha ya Kila Siku, nyimbo 12 ziliteuliwa kimakusudi kutoka nyimbo 30 alizoimba kati ya 2020 na 2025, kwa kuzingatia utajiri wa maudhui, mbinu za lugha za kisanaa na dhima ya kijamii. Nyimbo hizo zilisikilizwa zaidi ya mara moja, zikatafsiriwa kutoka Kijaluo kwenda Kiswahili, na data zikachanganuliwa kimaudhui kwa kufuata hatua za Braun na Clarke (2006). Matokeo yalibainisha maudhui matano makuu yanayoingiliana: mapenzi na uhusiano wa kimahaba; imani na utegemezi kwa Mungu; wivu, dharau na uvumilivu wa kijamii; ndoa, mahari na heshima ya familia; pamoja na falsafa ya maisha ya mara moja. Matokeo yanaonesha kuwa nyimbo hizi huakisi uzoefu wa maisha ya jamii ya Waluo huku zikiunganisha vipengele vya kimila na vya kisasa. Utafiti unapendekeza uchunguzi wa nyimbo za wasanii wengine wa *Ohangla* na wa maudhui ya kiimani kwa mitazamo ya kiteolojia au kiishara. Kwa ujumla, makala inaonesha mchango wa muziki wa asili katika kuwasilisha uzoefu wa kijamii na kiutamaduni katika enzi ya majukwaa ya kidijitali.

**Maneno Muhimu**: Jamii, maudhui, nyimbo za *Ohangla*, uhalisia, Waluo.

Editon OPEN ACCESS

This article is distributed under the license of a Creative Commons Attribution-Non Commercial-ShareAlike 4.0 International License. It is permitted to be used, reproduced and distributed in line with Editon Consortium Publishing guidelines.

## UTANGULIZI

Muziki wa *Ohangla* ni mojawapo ya tanzu maarufu za muziki wa asili nchini Kenya. Hata hivyo, bado kuna pengo katika uchunguzi wa kina wa maudhui ya nyimbo za kisasa za *Ohangla* za msanii mmoja kwa mtazamo wa kinadharia unaoeleza uhalisia wa maisha. Hilo ndilo tatizo linaloshughulikiwa na makala hii. Abrams na Harpham (2012) wanafafanua maudhui kama mawazo, hisia na uzoefu wa kijamii anaowasilisha msanii kupitia kazi yake. *Ohangla* ni densi na muziki wa asili wa jamii ya Waluo wa ukanda wa Ziwa Victoria. Kwa mujibu wa vyanzo vilivyotumiwa katika makala hii, muziki huo umehusishwa na maendeleo ya muziki wa Benga na umejenga sura yake kupitia ala kama ngoma ya *Ohangla*, nyatiti na orutu (Ogude, 2012; Okong'o, 2011). Nadharia ya Uhalisia, inayoongoza makala hii, inalenga kuwasilisha maisha ya binadamu kama yanavyojitokeza katika ulimwengu halisi, bila kupotosha wala kupamba ukweli (Abrams na Harpham, 2012).

Kihistoria, *Ohangla* iliimbwa katika harusi, mazishi ya wazee na karamu za kijiji, na iliwasilisha masuala ya mapenzi, siasa na maisha ya kijamii kwa jamii ya Waluo. Leo, muziki huu umebadilika kwa kiasi kikubwa kupitia wasanii kama Prince Indah (jina halisi Evans Ochieng' Owino), anayechanganya midundo asilia na Afrobeat pamoja na Reggae. Kazi zake husambazwa kupitia YouTube, TikTok na Instagram, hivyo kuvuka mipaka ya jamii ya Waluo pekee (Ochieng', 2022). Anatumia kwa wingi lugha ya Kijaluo na maudhui yanayogusa maisha ya jamii yake.

Tafiti zilizopo zinaonesha uwepo wa pengo hili. Anudo na Awuor (2017) alichunguza sitiari katika muziki wa *Ohangla* kwa kutumia Nadharia ya Pragmatiki, bila kumlenga msanii mmoja au kuchanganua maudhui kwa upana. Ogude (2012) alishughulikia historia na mabadiliko ya muziki wa jadi katika mazingira ya mijini, bila kuchanganua kimaudhui nyimbo za msanii mmoja. Awuor (2025) alijikita katika nyimbo za *Ohangla* za kidini, hivyo kuacha nafasi ya kuchunguza kwa upana nyimbo za kilimwengu za Prince Indah zinazohusu mapenzi, imani, mahusiano na maisha ya kila siku. Omolo-Ongati (2006) na Omondi Oduor na wenzake (2022) walichunguza *Ohangla* katika muktadha wa mabadiliko ya utendaji na mitazamo ya kijinsia, bila kulenga uchanganuzi wa kimaudhui wa nyimbo za msanii mmoja. Kwa mujibu wa mapitio haya, haijabainika utafiti unaotumia Nadharia ya Uhalisia kuchanganua nyimbo za *Ohangla* za Prince Indah katika kipindi cha 2020–2025. Pengo hili la kimaudhui, kinadharia na kimuktadha ndilo linalolengwa na makala hii.

Makala hii inawasilisha matokeo ya lengo la kwanza la utafiti mpana zaidi kuhusu nyimbo za *Ohangla* za Prince Indah. Inajibu swali: Ni maudhui yapi yanajitokeza katika nyimbo teule za Prince Indah, na yanaakisije uhalisia wa maisha ya jamii ya Waluo? Kwa kutumia Nadharia ya Uhalisia, hususan Mhimili wa Uhalisia wa Maisha ya Kila Siku, makala inabainisha maudhui matano makuu yanayoingiliana katika nyimbo za msanii huyu. Matokeo haya yanachangia uelewa wa jinsi muziki wa asili wa Kiafrika unavyoendelea kuakisi uhalisia wa maisha ya jamii katika enzi ya majukwaa ya kidijitali.

## MAPITIO YA MAANDISHI

Uchambuzi wa maudhui katika nyimbo na mashairi ni uwanja unaojadiliwa katika tafiti mbalimbali. Watafiti wameweka misingi ya kinadharia na kimethodolojia ya kuelewa jinsi maudhui yanavyowasilishwa katika kazi za muziki. Sehemu hii inapitia tafiti hizo kwa muktadha, kuanzia maudhui ya nyimbo za Kiafrika na kimataifa, muziki na utamaduni, muziki wa kisasa wa Afrika Mashariki, hadi tafiti mahususi kuhusu *Ohangla*.

### Maudhui ya Nyimbo za Kiafrika na za Kimataifa

Kwa mtazamo wa kimataifa, Kwon na wenzake (2021) walifanya uchambuzi wa kimfumo wa maudhui mazuri, mabaya na ya kawaida katika nyimbo maarufu za 1998–2018. Walibaini kuwa nyimbo hizo zinashughulikia mapenzi, familia, nguvu ya kijamii na hali za kiuchumi. Maudhui hayo yana athari kubwa kwa mtazamo wa wasikilizaji, hasa vijana. Utafiti huu unachangia utafiti wa sasa kwa kuonesha mbinu za kisayansi za kuainisha maudhui hususan uchambuzi wa maudhui, mbinu iliyotumika pia hapa. Tofauti ni kwamba wao walizingatia nyimbo za Magharibi kwa miaka ishirini na mtazamo mpana wa kiidadi. Kwa upande wake, utafiti huu unachunguza nyimbo za *Ohangla* za Prince Indah katika muktadha wa Kiafrika na Kiswahili, kwa kipindi kifupi cha miaka mitano (2020–2025). Utafiti huu utaangazia pengo lililoachwa na Kwon na wenzake, kwani hawakuchunguza kwa kina maudhui ya nyimbo za Kiafrika wala kuzingatia muktadha wa kikabila na kitamaduni.

Kwa mtazamo wa Kiafrika, Forchu (2020) alichunguza Hip Hop ya Kiigbo nchini Nigeria, akimtumia Phyno kama kielelezo. Alibaini maudhui ya utambulisho wa

kikabila, masuala ya kijamii na mapambano ya kiuchumi, yaliyowasilishwa kupitia sarufi na muundo wa kisanaa. Vile vile, Onanuga na Onanuga (2020) walibainisha maudhui makuu ya Hip Hop ya Nigeria, yakiwemo umaskini, ufisadi wa kisiasa, utambulisho wa Kiafrika na matarajio ya vijana. Walihitimisha kuwa nyimbo za Kiafrika zinaweza kusomwa kama hati za kijamii na kihistoria. Ngobili (2021) alitoa mapitio ya karibu miaka mia moja ya muziki maarufu wa Nigeria (1922–2020), akionesha jinsi maudhui yalivyobadilika kulingana na wakati. Tafiti hizi zinaonesha uwezo wa nyimbo za Kiafrika kuakisi hali za jamii. Hata hivyo, zimejikita zaidi katika muziki maarufu wa Afrika Magharibi, hasa Hip Hop ya Nigeria. Kwa hiyo, bado kuna nafasi ya kuchunguza muziki asilia wa Afrika Mashariki, hususan *Ohangla*, kwa kumlenga msanii mmoja na kutumia Nadharia ya Uhalisia. Makala hii inalenga kuziba pengo hilo kwa kuchunguza maudhui katika nyimbo 12 za Prince Indah.

**Muziki, Utamaduni na Jamii**

Mkallyah (2022) alichunguza nyimbo za watoto kama chombo cha kujifunza Kiswahili huko Dar es Salaam. Alionesha kuwa nyimbo hizo zina maudhui ya kielimu, kijamii na kiutamaduni yanayosaidia ujifunzaji. Ogutu na Githinji (2025) walifanya utafiti wa kiethnografia kuhusu jinsi nyimbo na sanaa za Kiswahili zinavyohifadhi kumbukumbu ya utamaduni katika Kisiwa cha Lamu. Walibaini kuwa maudhui ya nyimbo hizo yanahusisha historia, utamaduni, imani na maadili. Tafiti hizi zinaonesha kuwa nyimbo za kiasili hubeba thamani za kiutamaduni. Hata hivyo, hazijachunguza nyimbo za kiasili za Waluo kwa mtazamo unaolenga maudhui ya msanii mmoja. Makala hii inaangazia pengo hilo katika nyimbo za *Ohangla* za Prince Indah.

**Muziki wa Kisasa wa Afrika Mashariki**

Waswala na wenzake (2023) walitathmini nyimbo za mazingira za kisasa za Kiswahili. Walibaini maudhui kama uhifadhi wa mazingira, athari za mabadiliko ya tabianchi, na jukumu la binadamu katika kulinda mazingira. Utafiti huu unaonesha kuwa muziki wa kisasa wa Afrika Mashariki unaweza kubeba maudhui yanayohusu masuala ya sasa. Tofauti inayojitokeza ni kwamba wao walilenga maudhui ya mazingira, ilhali makala hii inachunguza maudhui mbalimbali yanayoingiliana katika nyimbo za msanii mmoja. Kwa hiyo, utafiti huu unaongeza muktadha wa *Ohangla* kama muziki wa asili wa Waluo unaosambazwa pia kupitia majukwaa ya kidijitali.

**Tafiti Kuhusu *Ohangla***

Anudo na Awuor (2017) katika tasnifu yao ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Nairobi, alishughulikia moja kwa moja muziki wa *Ohangla*. Kwa kutumia Nadharia ya Pragmatiki, alichunguza sitiari katika muziki wa *Ohangla* na kubaini aina mbalimbali zinazobeba maudhui ya kijamii, kisiasa na kiutamaduni ya jamii ya Waluo. Kazi hii ni msingi muhimu kwa utafiti huu kwa sababu inalenga moja kwa moja *Ohangla*. Hata hivyo, Anudo na Awuor (2017) walitumia nadharia tofauti na Uhalisia na hakumlenga msanii mmoja wala kuchanganua maudhui ya nyimbo zake kwa upana. Makala hii, kwa upande wake, inamlenga Prince Indah na kuchanganua maudhui yanayojitokeza katika nyimbo 12 teule.

Kwa jumla, tafiti zilizopitiwa zinaonesha kuwa maudhui ya nyimbo za Kiafrika yamepata umakini wa kitaaluma. Hata hivyo, nyingi zimeegemea muziki wa Afrika Magharibi au muziki maarufu, kwa mtazamo mpana wa kikanda. Bado kuna pengo katika uchanganuzi wa kina wa nyimbo za msanii mmoja wa *Ohangla* kwa kipindi maalum cha 2020–2025 na kwa kutumia Nadharia ya Uhalisia. Makala hii inalenga kuziba pengo hilo kwa kutoa uchanganuzi wa kimaudhui wa nyimbo 12 za Prince Indah.

**Misingi ya Nadharia**

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uhalisia, iliyoibuka Ufaransa kati ya miaka 1830 na 1850 ikiasisiwa na waandishi kama Honoré de Balzac na Gustave Flaubert, kabla ya kupanuka Uingereza kupitia Charles Dickens na George Eliot, na Marekani kupitia Mark Twain na Henry James (Lukács, 1971). Kwa mujibu wa Abrams na Harpham (2012), Nadharia ya Uhalisia ni mfumo wa kinadharia unaolenga kuwasilisha maisha ya binadamu kama yanavyoonekana katika ulimwengu halisi, bila kupamba wala kupotosha ukweli, ikiepuka usimulizi wa kimapenzi au wa kufikirika.

Nadharia hii ina mihimili sita: Uhalisia wa Maisha ya Kila Siku, Ukweli wa Kisaikolojia, Uamuzi wa Kitabaka na Kijamii, Usimulizi wa Lengo, Uteuzi Makini wa Maelezo, na Uakisi wa Mazingira ya Wakati Maalum. Kila mhimili unashughulikia kipengele tofauti cha uwakilishi wa uhalisia. Nadharia hii ilichaguliwa kwa sababu inatoa msingi wa kutathmini namna kazi ya kisanaa inavyowasilisha uzoefu wa maisha halisi. Katika makala hii, uchanganuzi umejikita mahsusi katika

maudhui, kwa kuongozwa na Mhimili wa Uhalisia wa Maisha ya Kila Siku.
Kwa lengo la kwanza linalowasilishwa katika makala hii, mhimili ulioongoza uchanganuzi ni Uhalisia wa Maisha ya Kila Siku. Mhimili huu unasisitiza kwamba kazi ya kisanaa inaweza kuakisi hali halisi za maisha, ikiwemo mazungumzo ya kawaida, matatizo ya kimwili, kiuchumi na kijamii. Kwa mujibu wa Becker (1963), uhalisia wa kifasihi huzingatia uzoefu unaoweza kutambuliwa katika maisha badala ya kutegemea fikira za kufikirika pekee. Kanuni hii iliongoza mtafiti kutathmini kama maudhui yanayojitokeza katika wimbo yanaakisi uzoefu unaotambulika wa jamii ya Waluo, kama vile mapenzi, imani, wivu, ndoa na ufupi wa maisha.

Kigezo cha pili kilichoongoza uchanganuzi kilikuwa kujitokeza kwa dhamira husika katika zaidi ya wimbo mmoja miongoni mwa nyimbo 12 teule. Kujitokeza kwa dhamira katika nyimbo kadhaa kulisaidia kutofautisha mifumo ya maudhui na matukio yaliyotokea katika wimbo mmoja pekee. Vigezo hivi viwili—uhalisia wa uzoefu na kujirudia kwa dhamira—viliongoza uainishaji wa data katika uchanganuzi wa kimaudhui.

## MBINU ZA UTAFITI

Utafiti ulitumia muundo wa kimaelezo wa kitaamuli. Creswell na Poth (2018) wanaeleza kuwa utafiti wa kitaamuli husaidia kueleza na kufasiri maana za matukio kwa kutumia data za kimaelezo. Muundo huu ulifaa kwa sababu utafiti ulilenga kutambua na kufasiri maudhui yanayojitokeza katika nyimbo teule za *Ohangla*.

Eneo la utafiti lilikuwa nyimbo za *Ohangla* za Prince Indah zilizohifadhiwa kwenye YouTube, ambazo zilikuwa chanzo kikuu cha data ya msingi. Data ya sekondari ilipatikana katika vitabu, majarida na tasnifu zinazohusiana na mada. Kikundi lengwa kilikuwa nyimbo 30 alizoimba Prince Indah kati ya 2020 na 2025, kati ya zaidi ya nyimbo 90 alizotoa tangu 2014. Idadi hii ilithibitishwa kwa kuorodhesha video zilizopakiwa kwenye kituo rasmi cha YouTube cha msanii, "*Malaika Ohangla Rhumba*", kati ya Januari 2020 na Desemba 2025. Mtafiti alizihakiki dhidi ya tarehe za kupakiwa ili kuondoa nyimbo zilizorudiwa. Ufikiaji wa data ulifanyika Aprili hadi Julai 2026.

Kutokana na idadi ya nyimbo zilizobainishwa, mtafiti alitumia usampulishaji wa kimakusudi kuteua nyimbo 12 kati ya 30. Vigezo vya uteuzi vilikuwa utajiri wa maudhui, mbinu za lugha za kisanaa, athari, na dhima kwa wanajamii. Patton (1990) anasisitiza umuhimu wa sampuli yenye kina katika utafiti wa kitaamuli. Nyimbo 12 zilitoa uwiano kati ya upana na kina cha uchanganuzi na zilitoa utofauti wa kimaudhui unaohusiana na lengo la utafiti.

Mtafiti alisikiliza nyimbo hizo kwa makini zaidi ya mara moja na kudondoa data muhimu katika daftari. Kisha alitafsiri maneno ya nyimbo kutoka Kijaluo kwenda Kiswahili kwa kuzingatia misingi ya usawe (Nida na Taber, 1982). Lengo lilikuwa kuhifadhi maana na ujumbe wa nyimbo bila kuwapotosha.

Uchanganuzi wa data ulifuata hatua za uchanganuzi wa mada za Braun na Clarke (2006). Mtafiti alijifahamisha na data kwa kuzisikiliza nyimbo mara kwa mara, akazalisha misimbo ya awali, akatafuta mada zilizojitokeza, akazipitia na kuzifafanua, kisha akazipa majina. Data ziliainishwa kulingana na mada zilizobainika na kufasiriwa kwa kuzingatia Mhimili wa Uhalisia wa Maisha ya Kila Siku. Madondoo mafupi kutoka katika nyimbo yalitumiwa kama ushahidi wa uchanganuzi na kujadiliwa kwa kurejelea tafiti zilizotangulia.

Kimaadili, mtafiti alipata kibali rasmi kutoka Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki na idhini kutoka NACOSTI kabla ya kuanza ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Utafiti uliheshimu haki ya kiutunzi ya Prince Indah, na kila dondoo kutoka katika nyimbo zake lilitambuliwa kama kazi yake ya ubunifu na kutumiwa kwa madhumuni ya kitaaluma. Usahihi wa tafsiri ulizingatiwa ili kuepuka kupotosha maana ya maneno ya msanii.

## MATOKEO NA MAJADILIANO

Uchanganuzi wa nyimbo 12 teule za Prince Indah ulibainisha maudhui matano makuu yanayoingiliana na kutegemeana, kama inavyooneshwa katika Jedwali 1. Ushahidi wa kila maudhui unawasilishwa katika sehemu hii na kufasiriwa zaidi katika Majadiliano.

**Jedwali 1: Muhtasari wa Maudhui Yanayojitokeza katika Nyimbo Teule za *Ohangla* za Prince Indah**

| Maudhui | Maelezo mafupi | Nyimbo husika |
|---|---|---|
| Mapenzi na uhusiano wa kimahaba | Mapenzi matamu ya awali, mashaka na wivu, maumivu ya kuvunjika kwa uhusiano, usaliti, na undani wa mapenzi ya kimwili. | 1, 2, 3, 4, 7, 8, 9, 10, 11 |
| Imani na utegemezi kwa Mungu | Shukrani kwa Mungu kwa mafanikio, uhusiano binafsi na Mungu kama msingi wa kujiamini dhidi ya dharau, rejeleo za kibiblia, na imani kama kimbilio la faraja. | 1, 3, 5, 8, 11, 12 |
| Wivu, dharau na uvumilivu wa kijamii | Kukejeliwa kabla ya kufanikiwa, sitiari za kuwafichua wanafiki, hatua za kukabiliana na dharau, na wivu wa kimapenzi unaotokana na mitandao ya kijamii. | 1, 5, 6, 9, 11, 12 |
| Ndoa, mahari na heshima ya familia | Ahadi ya kulipa mahari, wazee kuitwa kutatua migogoro ya kifamilia, msamiati wa heshima wa kimila, na taratibu za kumpeleka mpenzi nyumbani kwa wazazi. | 1, 3, 4, 9, 10 |
| Falsafa ya maisha ya mara moja | Kuhimiza kufurahia maisha sasa, ombi la kupendwa kwa dharura kwa sababu ya uhai, wajibu wa kutumia muda vizuri, na ubatili wa wivu ndani ya muda mfupi wa maisha. | 2, 5, 9, 10, 12 |

**Maudhui ya Mapenzi na Uhusiano wa Kimahaba**

Maudhui ya mapenzi ndiyo yanayoongoza katika nyimbo teule, yakijitokeza katika nyimbo 9 kati ya 12 kwa sura mbalimbali: uchumba mtamu wa awali, mashaka na wivu, maumivu ya kuvunjika kwa uhusiano, usaliti, na undani wa mapenzi ya kimwili. Katika Wimbo wa Kwanza, msanii anaelezea uchungu wa kutengana kwa swali la kihisia:

*"Akoni lit to lit nyathi jomoko chieng' ayuag ne ng'a?"*
*(Nakuambia kweli ni chungu mwana wa wenyewe nitamlilia nani?)*

*(Wimbo 1: Kwach Ogolo Koke, Prince Indah, 2020–2025).*

Swali hili linarudiwa mara tatu mfululizo kwa maneno yanayotofautiana kidogo. Wimbo wa Nne, "*Jatuka*", unaongeza wivu wa aina mbili: wivu wa ana kwa ana na wivu wa kiteknolojia unaotokana na simu isiyopokewa.

Aidha, Wimbo wa Nane, *"Kogik Otieno"*, unawasilisha undani wa mapenzi ya kimwili kati ya wapenzi wawili wanaotamani ukaribu wakati wa usiku, hamu inayosisitizwa kupitia takriri ya mfululizo mwanzoni mwa wimbo:

*"Bing'e nagombo kogik otieno oooh"*
*(Unajua ninatamani usiku ukifika oooh)*

*(Wimbo 8: Kogik Otieno, Prince Indah, 2020–2025).*

**Maudhui ya Imani na Utegemezi kwa Mungu**

Nyimbo kadhaa za Prince Indah zinaakisi imani thabiti ya kidini na utegemezi kwa Mungu katikati ya changamoto za maisha. Katika Wimbo wa Tano, "*Girwa Ni*", msanii anaeleza jinsi anavyoshukuru Mungu kwa mafanikio yake huku akiwaonya wanaomkejeli:

*"An gimang'eyo ni ruoth ogenaa"*
*(Ninachojua ni kwamba Mungu ananithamini)*

*(Wimbo 5: Girwa Ni, Prince Indah, 2020–2025).*

Wimbo wa Kumi na Mbili, "*Ngima Dhano*", unarejelea moja kwa moja Zaburi ya 23. Katika nyimbo 6 kati ya 12, rejeleo la Mungu linajitokeza kama sehemu ya maudhui ya imani na utegemezi kwake. Hata hivyo, maudhui ya kiimani yanaingiliana pia na maudhui mengine, kama wivu, mafanikio na falsafa ya maisha.

**Maudhui ya Wivu, Dharau na Uvumilivu wa Kijamii**

Maudhui haya yanaonesha jinsi msanii anavyokabiliana na dharau, wivu na kejeli kutoka kwa jamii kutokana na mafanikio yake. Katika Wimbo wa Tano, msanii anatumia sitiari ya fisi waliovaa mavazi ya kondoo kuwafichua wanafiki wanaomsengenya kwa siri:

*"Girwako kode rombe to mana ondiegii"*
*(Wanavaa mavazi ya kondoo, kumbe ni fisi tu)*

*(Wimbo 5: Girwa Ni, Prince Indah, 2020–2025).*

Wimbo wa Sita, "*Osiepe*", unaonesha mabadiliko ya hadhi ya kijamii kutoka kudharauliwa hadi kuitwa rafiki, hali inayowasilishwa kama inayohusiana na hali ya kiuchumi ya mtu badala ya thamani yake ya asili.

**Maudhui ya Ndoa, Mahari na Heshima ya Familia**

Maudhui ya taasisi ya ndoa na desturi za kimila za Kiluo, kama mahari na baraza la wazee, yanajitokeza kwa uwazi katika Wimbo wa Kwanza, ambapo msanii anaahidi kulipa mahari maradufu endapo atashindwa kesi ya kimahakama dhidi ya mpenzi wake, huku akitaja mashahidi mahususi wakiwemo wazee na kiongozi wa kidini. Wimbo wa Tatu, "*Mama Watoto*", unaonesha shauku ya msanii ya kumfanya mpenzi wake kuwa mke rasmi, akitumia neno la heshima la kimila:

*"Kik bed naleko lek ma pok ochoponi yuora"*
*(Isiwe kwamba ninaota ndoto ambayo haijakutimilia, shemeji)*

*(Wimbo 3: Mama Watoto, Prince Indah, 2020–2025).*

Neno "shemeji" linajitokeza tena katika Wimbo wa Tisa na wa Kumi. Kujirudia huku kunaashiria umuhimu wa msamiati wa heshima wa kifamilia katika kuwasilisha mahusiano ya kimapenzi na matarajio ya ndoa.

**Maudhui ya Falsafa ya Maisha ya Mara Moja**

Nyimbo za Pili, Tano, Tisa, Kumi na Kumi na Mbili zinabeba falsafa ya kuishi maisha kwa ukamilifu kwa kuzingatia wazo kwamba binadamu huishi mara moja tu duniani. Katika Wimbo wa Pili, msanii anahimiza kufurahia maisha na mapenzi:

*"Piny idake dichiel ma e kindewa"*
*(Duniani mtu huishi mara moja huu ndio wakati wetu)*

*(Wimbo 2: Nyar Joluo, Prince Indah, 2020–2025).*

Wimbo wa Tano unaongeza sura ya kimaadili kwa falsafa hii: ufupi wa maisha si sababu ya kuachilia kila kitu bila mpangilio, bali ni sababu ya kutumia kwa busara rasilimali za muda, nguvu na pesa chini ya uangalizi wa Mungu. Wimbo wa Kumi, "*Rembo*", unaongeza kipengele cha dharura kwa falsafa hiyo hiyo, msanii akiomba apendwe kwa sababu bado yuko hai; kirai hicho kinarudiwa mara kadhaa wimboni humo kikiambatana na majina tofauti ya wapenzi.

**Majadiliano**

Sehemu hii inatafsiri matokeo yaliyowasilishwa hapo juu, ikiyahusisha na mihimili ya Nadharia ya Uhalisia pamoja na tafiti za awali, ili kubainisha uzito wake wa kitaaluma.

**Mapenzi na Uhusiano wa Kimahaba**

Msanii anawasilisha mapenzi kama mchakato wenye hatua na hisia tofauti, jambo linaloendana na Mhimili wa Uhalisia wa Maisha ya Kila Siku. Wivu wa aina mbili unaojitokeza katika Wimbo wa Nne unaonesha kuwa wasiwasi wa kimapenzi unahusisha mahusiano ya ana kwa ana na yale yanayoathiriwa na teknolojia ya mawasiliano. Mchanganyiko huu wa masuala ya kimapenzi na teknolojia unaunga mkono uchunguzi wa Wanjala na Kebaya (2016) kuhusu nyimbo maarufu za Kenya za kisasa. Kadhalika, Kwon na wenzake (2021) walibaini kuwa mapenzi ni miongoni mwa maudhui yanayojitokeza kwa wingi katika muziki maarufu, jambo linaloweka matokeo ya Prince Indah katika muktadha mpana wa muziki.

Wimbo wa Nane unajikita katika hamu ya kimwili ya ukaribu na kuiwasilisha kwa uwazi. Uwasilishaji huu unaendana na hoja ya Fadipe na Salawu (2022) kuhusu namna baadhi ya nyimbo maarufu za Kiafrika zinavyoshughulikia mada za mapenzi ya kimwili.

**Imani na Utegemezi kwa Mungu**

Kauli ya Wimbo wa Tano inaonesha jinsi msanii anavyowasilisha kujiamini kupitia uhusiano wake na Mungu badala ya kutegemea maoni ya jamii. Rejeleo la Zaburi ya 23 katika Wimbo wa Kumi na Mbili linaonesha matumizi ya hazina ya pamoja ya kidini inayoweza kutambulika na hadhira. Uwepo wa lugha ya kiimani ndani ya nyimbo za kilimwengu unaendana na uchunguzi wa Ogutu na Githinji (2025) kuhusu historia, utamaduni na imani katika nyimbo za Kiswahili, pamoja

na Van der Merwe na Morelli (2022) kuhusu uhusiano kati ya ushiriki wa muziki na hisia ya kuwa sehemu ya jamii.

**Wivu, Dharau na Uvumilivu wa Kijamii**

Masimulizi ya "kutoka dharauni hadi mafanikioni" yanayojitokeza katika Wimbo wa Tano na wa Sita yanaweza kuwekwa katika muktadha mpana wa muziki maarufu wa Kiafrika (Forchu, 2020). Mzunguko wa hadhi ya kijamii unaoonekana katika Wimbo wa Sita, "*Osiepe*", unaendana na mjadala wa muziki wa *Ohangla* kama jukwaa la kuwasilisha uzoefu wa kijamii. Uvumilivu unaodhihirishwa katika nyimbo hizi unaunganishwa pia na maudhui ya imani, hivyo kuonesha mwingiliano wa maudhui katika data.

**Ndoa, Mahari na Heshima ya Familia**

Muungano wa kimila na usasa, unaoonekana katika msamiati na taratibu zilizowasilishwa hapo juu, unaunga mkono hoja ya Omondi Oduor na wenzake (2022) kwamba maonyesho ya *Ohangla* yanaendelea kuimarisha mitazamo ya kimila ya kijinsia na kifamilia miongoni mwa jamii ya Waluo, hata pale wasanii wanapotumia majukwaa ya kisasa kama YouTube kusambaza ujumbe huo.

**Falsafa ya Maisha ya Mara Moja**

Falsafa ya kuishi maisha kwa ukamilifu inayojitokeza katika nyimbo za Pili, Tano, Tisa, Kumi na Kumi na Mbili inaendana na msingi wa Auerbach (2003) kwamba sanaa ya kiuhalisia inaweza kuakisi hali za kawaida za uwepo wa binadamu, ikiwemo ufupi wa maisha. Hata hivyo, uhusiano wa falsafa hii na hali ngumu za kiuchumi za vijana wa Kenya unahitaji ushahidi wa moja kwa moja zaidi kuliko uliotolewa katika data hii; kwa hiyo, makala hii inaichukulia kama tafsiri inayowezekana, si hitimisho la moja kwa moja. Uunganisho wa falsafa ya maisha na maudhui ya imani na wivu katika baadhi ya nyimbo unaonesha kuwa maudhui madogo yanaingiliana na kutegemeana.

**Muhtasari wa Majadiliano**

Kwa jumla, matokeo yanaendana na tafiti zilizotangulia zinazoonesha kuwa mapenzi, familia, imani na masuala ya kijamii ni miongoni mwa maudhui yanayoweza kujitokeza katika muziki wa Kiafrika. Hata hivyo, makala hii inaonesha namna maudhui hayo yanavyounganishwa katika nyimbo za msanii mmoja wa *Ohangla* na kuhusishwa na uzoefu wa maisha ya jamii ya Waluo. Matokeo haya yanaongeza muktadha wa *Ohangla* katika mjadala wa muziki wa asili wa Afrika Mashariki na uwasilishaji wake kupitia majukwaa ya kidijitali.

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

**Hitimisho**: Makala hii ilibainisha maudhui matano makuu yanayoingiliana katika nyimbo teule za *Ohangla* za Prince Indah: mapenzi na uhusiano wa kimahaba; imani na utegemezi kwa Mungu; wivu, dharau na uvumilivu wa kijamii; ndoa, mahari na heshima ya familia; pamoja na falsafa ya maisha ya mara moja.

Mhimili wa Uhalisia wa Maisha ya Kila Siku ulitoa msingi wa kuchanganua namna maudhui haya yanavyohusishwa na uzoefu wa maisha ya jamii ya Waluo, ukiwemo mahusiano ya kisasa, taratibu za kimila kama mahari, changamoto za kijamii na ufupi wa maisha. Hata hivyo, uchanganuzi unaonesha kuwa mhimili huu pekee hauwezi kueleza kikamilifu vipengele vya kiimani, hasa rejeleo za kibiblia na maana zake za kiishara. Hivyo, uchunguzi wa maudhui ya imani unaweza kunufaika na mtazamo wa ziada wa kiteolojia au kiishara. Aidha, mwingiliano wa maudhui katika wimbo mmoja unaonesha kuwa nyimbo hizi haziwezi kila mara kugawanywa katika kategoria zinazojitegemea kabisa.

Matokeo ya makala hii yanaonesha kuwa tafiti zilizopo zimeelekea kuangazia maudhui ya muziki wa Kiafrika kwa mtazamo mpana wa kikanda au kimataifa, huku uchanganuzi wa kina wa nyimbo za msanii mmoja wa *Ohangla* ukiwa bado na nafasi ya kuendelezwa. Makala hii inaongeza uelewa wa namna Nadharia ya Uhalisia inavyoweza kutumika kuchanganua maudhui ya muziki wa asili wa Kiafrika. Hata hivyo, matokeo haya yanapaswa kueleweka ndani ya mipaka ya sampuli ya nyimbo 12 za msanii mmoja na kipindi cha 2020–2025.

**Mapendekezo**

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, tunapendekeza tafiti za baadaye zichunguze nyimbo za wasanii wengine wa *Ohangla* ili kubaini iwapo muundo huu wa maudhui yanayoingiliana ni sifa pana ya muziki wa *Ohangla* au unahusishwa zaidi na Prince Indah. Vilevile, tafiti zijazo zinaweza kuchunguza kwa kina maudhui ya imani katika nyimbo za *Ohangla* kwa kutumia mitazamo ya kiteolojia au kiishara, ili kukamilisha vipengele ambavyo Nadharia ya Uhalisia haiwezi kuvieleza kikamilifu. Matokeo haya pia yanaweza kutumiwa kama msingi wa kuandaa nyenzo za kufundishia fasihi simulizi ya Kiswahili na Kijaluo katika elimu ya juu.

**MAREJELEO**

Abrams, M. H., & Harpham, G. G. (2012). *A glossary of literary terms* (10th ed.). Wadsworth Cengage Learning.

Auerbach, E. (2003). *Mimesis: The representation of reality in Western literature* (W. R. Trask, Trans.). Princeton University Press. (Original work published 1946)

Awuor, E. Q. (2025). Multilingual communication strategies in African religious music: A linguistic study of Dholuo Ohangla gospel expression. *Journal of Linguistics, Literary and Communication Studies, 4*(2), 80–91. https://doi.org/10.58721/jllcs.v4i2.1236

Ayinla Fadipe, I., & Salawu, A. (2022). "Coronavirus, you are a stranger": Examining Yoruba indigenous music in the quest to tackle COVID-19 pandemic. *Journal of African Films and Diaspora Studies, 5*(1), 75–99. https://doi.org/10.31920/2516-2713/2022/5n1a4

Becker, G. J. (1963). *Documents of modern literary realism*. Princeton University Press.

Braun, V., & Clarke, V. (2006). Using thematic analysis in psychology. *Qualitative Research in Psychology, 3*(2), 77–101. https://doi.org/10.1191/1478088706qp063oa

Creswell, J. W., & Poth, C. N. (2018). *Qualitative inquiry and research design: Choosing among five approaches* (4th ed.). SAGE Publications.

Forchu, I. I. (2020). Rhythmic idioms in Igbo hip hop music: Phyno as exemplar. *Journal of the Musical Arts in Africa*, *17*(1), 19–40. https://doi.org/10.2989/18121004.2020.1851458

Kwon, L., Medina, D., Ghattas, F., & Reyes, L. (2021). Trends in positive, negative, and neutral themes of popular music from 1998 to 2018: Observational study. *JMIR Pediatrics and Parenting, 4*(2), e26475. https://doi.org/10.2196/26475

Lukács, G. (1971). *The historical novel* (H. Mitchell & S. Mitchell, Trans.). Penguin Books.

Mkallyah, K. A. (2022). Songs and language: Children's songs and the learning of Kiswahili in Dar es Salaam, Tanzania. *Umma Journal of Contemporary Literature and Creative Arts, 9*(2). https://journals.udsm.ac.tz/index.php/umma/article/view/5386

Ngobili, C. (2021). Close to a century of popular music practices and experiences in Nigeria (1922–2020) and a brief history of their socio-political background. *Muziki, 18*(1), 34–58. https://doi.org/10.1080/18125980.2021.1958696

Nida, E. A., & Taber, C. R. (1982). *The theory and practice of translation*. E. J. Brill.

Ochieng', P. (2022). *The origin and transformation of Ohangla music in Siaya County, Kenya* [Unpublished manuscript]. University of Nairobi.

Ogude, J. (2012). The invention of traditional music in the city: Exploring history and meaning in urban music in contemporary Kenya. *Research in African Literatures*, *43*(4), 147–164. https://doi.org/10.2979/reseafrilite.43.4.147

Ogutu, W., & Githinji, P. (2025). Preserving the collective memory of the Swahili culture: An ethnographic study of Lamu Island. *East African Journal of Traditions, Culture and Religion, 8*(1), 188–200. https://doi.org/10.37284/eajtcr.8.1.3493

Okong'o, J. B. (2011). Ohangla music as a parodic genre and postcolonial Luo experience. *Africa Today, 57*(3), 23–44. https://doi.org/10.2979/africatoday.57.3.23

Omolo, H. O. (2020). *A lexical pragmatic approach to Ohangla music: A case of metaphors*. University of Nairobi. https://erepository.uonbi.ac.ke/items/8be0e540-1631-43f6-b26e-cd53a5239b0b

Omolo-Ongati, R. A. (2006). Change, innovation and continuity in the performance practice of traditional Luo instrumental genres in contemporary popular settings. In *Centering on African practice in musical arts education* (p. 141).

Omondi Oduor, J., Wako, F., & Walunywa, J. (2022). Ohangla performance as a vehicle for transforming gender consciousness among the Luo of Kenya. *Journal of Languages and Linguistics (JLL), 1*(1), 23–34. https://doi.org/10.51317/jll.v4i1.258

Onanuga, P. A., & Onanuga, A. O. (2020). Violence, sexuality and youth linguistic behaviour: An exploration of contemporary Nigerian youth music. *Contemporary Music Review, 39*(1), 137–166. https://doi.org/10.1080/07494467.2020.1753478

Patton, M. Q. (1990). *Qualitative evaluation and research methods* (2nd ed.). SAGE Publications.

van der Merwe, L., & Morelli, J. (2022). Explaining how community music engagement facilitates social cohesion through ritualised belonging. *Religions*, *13*(12), 1170. https://doi.org/10.3390/rel13121170

Wanjala, H., & Kebaya, C. (2016). Popular music and identity formation among Kenyan youth. *Muziki*, *13*(2), 20–35. https://doi.org/10.1080/18125980.2016.1249159

Waswala, B. O., Owiti, C. D., Jepkemei, F., & Kodak, B. (2023). An evaluation of contemporary East African Kiswahili environmental songs. *Cogent Arts & Humanities, 10*(2), Article 2289246. https://doi.org/10.1080/23311983.2023.2289246

Anudo, N. C., & Awuor, E. Q. (2017). Benga meets Ohangla: An analysis of animal metaphors used in selected Dholuo political songs. *International Journal of Science, Arts and Commerce*, *1*(12), 13–33. https://ir-library.kabianga.ac.ke/items/37019c5b-61c3-4d51-ab73-2208f6452178/fullir-library.kabianga.ac+1